

# **MIELEKEO YA WALIMU KUHUSU VITABU VYA KISWAHILI VYA MTALAA MPYA KATIKA SHULE ZA MSINGI**

**OWALA, J.A. (PhD)**

**CHUO KIKUU CHA RONGO**

**KITIVO CHA ELIMU NA SAYANSI YA JAMII**

**IDARA YA LUGHA, ISIMU NA FASIHI**

[jaelowala@gmail.com](mailto:jaelowala@gmail.com)

## **IKISIRI**

*Mtaala mpya umebuniwa nchini Kenya wa 2-6-3-3-3, ambapo wanafunzi wanatakiwa kusoma kwa miaka miwili katikashule ya chekechea, miaka sita katika shule ya msingi, miaka mitatu kwenye awamu ya chini ya shule ya upili, miaka mitatu kwenye awamu ya juu ya shule ya upili na miaka mitatu katika chuo kikuu. Walimu, kupitiataasisi ya kustawisha mtaala wa masomo nchini Kenya (KICD), wamehamasishwa kuhusu mchakato mzima. Mtaala huu una vifaa vyakemaalum ambavyovinapaswa kutumiwa kutekeleza malengo ya mtaala huu, na vifaa mojawapomuhimu ni vitabu vya kiada na miongozo ya walimu. Walimu ambao ni watekelezaji wa mtaala wanaweza kuwa na mielekeo tofautitofauti kuhusu vitabu hivi vya kiada ambavyo wanapaswa kutumia kufunza katika kutekeleza malengo ya mtaala huu. Baadhi ya maswali yatakayojibiwa katika utafiti huu ni je, mielekeo yao inaathiri vipi utekelezaji wa malengo ya mtaala huu? Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya utabia na data itakayotumiwa itakusanywa kutoka kwa walimuwa shule za msingi ambao wanapatikana katika gatuzi ndogo ya Marindi, kaunti ya Migori iliyo na shule nne za msingi.*